**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

## 1.0. Taarifa fupi ya Halmshauri ya Mji Kasulu

### Utangulizi

Halmashauri ya Mji Kasulu ni miongoni mwa Halmashauri nane zinazounda Mkoa wa Kigoma, Halmashauri nyingine ni Manispaa ya Kigoma/ Ujiji, Kigoma, Kibondo, Kasulu, Kakonko, Uvinza na Buhigwe. Halmashauri hii ilianzishwa mwaka 2011 kwa tangazo la Serikali Na 175 la tarehe 17 Juni 2011 na kuanza shughuli zake rasmi tarehe 1 Julai 2015. Kabla ya kuundwa, Halmashauri hii ilikuwa ni sehemu ya Halmashauri ya Wilaya Kasulu.

Eneo la Mji huu ni Kilometa za mraba 878.8 na imepakana na Halmshauri ya Wilaya Kasulu katika upande wa Mashariki, Kaskazini na Kusini na kwa upande wa Magharibi imepakana na Wilaya ya Buhigwe.

### Hali ya Hewa

Halmashauri ya Mji Kasulu ina hali ya hewa nzuri inayofaa kwa kilimo na ufugaji, hupata mvua kwa wastani 800 – 1800mm kwa mwaka na joto la wastani kati ya nyuzi Joto 26ºC -29ºC. Hali hii ya hewa hufaa kwa uzalishaji wa mazao mbalimbali.

### Idadi ya Watu

Kwa mujibu wa matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi iliyofanyika mwezi Agosti, 2012, Halmashauri ya Mji Kasulu ilikuwa na wakazi 208,244. (Wanaume 99,368. na Wanawake 108,876.). Kwa sasa, Halmashauri inakadiriwa kuwa na watu wapatao 245,851 (Wanaume 118,008 na Wanawake 127,843) ambapo ongezeko la watu kwa mwaka ni wastani wa asilimia 2.4.

### Muundo wa Utawala

Halmashauri ya Mji Kasulu imeundwa na Tarafa mbili (2) ambazo ni Heru Juu na Heru Chini, zikiwa na Kata 15 na Mitaa 108. Aidha, kuna Jimbo moja la uchaguzi ambalo ni Kasulu Mjini.

| Tarafa | Idadi ya Kata | Idadi ya Mitaa |
|---|---|---|
| HeruJuu | 3 | 27 |
| HeruChini | 12 | 81 |

## 2.0. MAPENDEKEZO YA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2020/2021.

**UTANGULIZI:**

**Mheshimiwa Mwenyekiti.**

Uandaaji wa Mpango na Bajeti kwa kila mwaka wa fedha ni hitaji la kikatiba. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 toleo la mwaka 2005 Ibara ya 145 (i) inataja kuwepo kwa Serikali za Mitaa na sheria ya Serikali za Mitaa namba 9 kifungu 43 ya mwaka 1982. Sheria zote hizo zinataja uwepo wa Serikali za mitaa na malengo ya kuwepo kwa Serikari za mitaa ni kupeleka madaraka kwa wananchi kwa kushiriki na kuwashirikisha wananchi katika mipango na shughuli za utekelezaji wa maendeleo.

**Mheshimiwa mwenyekiti,**

Katika kuandaa mpango huu mfumo wa upangaji Mipango Shirikishi Jamii wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (O&OD) umezingatiwa ambapo mipango shirikishi ilifanyika katika Mitaa 108 na kata zote 15. Mambo mengine yaliyozingatiwa katika kuandaa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ni pamoja na:-

1. Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21)
2. Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs)
3. Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ya Mwaka (2015-2020)
4. Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015 na Kanuni za Bajeti za mwaka 2015
5. Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akizindua Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 20 Novemba, 2015
6. Uwezo wa Bajeti wa Serikali kuu, Halmashauri na uwezo wa wananchi kuweza kuchangia miradi ya mandeleo katika maeneo yao.
7. Mwongozo wa maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2020/2021

Kuendelea **kufuata maelekezo muhimu kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa** kama yalivyotolewa kwenye Mwongozo wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2020/2021 kwa kuzingatia yafuatayo;-

a. Kujenga, kurekebisha na kuimarisha miundombinu ya jamii na kiuchumi hususan katika sekta za Elimu, Maji, Afya, Kilimo, Barabara, Mifugo na Uvuvi kwa kuzingatia ubora.
b. Kuwa na miradi michache inayotekelezeka na kukamilika mwishoni mwa mwaka.
c. Kuongeza mapato yanayokusanywa na Halmashauri yenyewe “Own Sources”.
d. Kupunguza matumizi katika matengenezo ya Magari, posho za semina na warsha.
e. Kuhakikisha malipo ya madeni mbalimbali ya Halmashauri na watumishi yanawekwa katika Bajeti.
f. Ununuzi wa samani uzingatie ubora wa bidhaa imara zinazozalishwa nchini.

## 2.1. MAPITIO YA UTEKELEZAJI MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

**Utangulizi**

Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Halmashauri ya Mji Kasulu ilikadiria kukusanya na kutumia jumla ya Tshs. **29,229,662,102.25** Fedha hizo zilitegemewa kutoka katika vyanzo vya Mapato ya Ndani, Serikali Kuu na Wafadhili kama jedwali hapo chini linavyoonesha.

**Jedwali 1: Makadirio ya bajeti na mapokezi ya Fedha katika Mwaka wa Fedha 2018/2019**

| Na | Chanzo cha Fedha | Makisio | Mapato Halisi | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Ndani yasiyo ya masharti | 1,361,198,600.0 | 1,029,602,344.13 | 75.64 |
| 2 | Mapato ya Ndani yenye Masharti | 424,090,000.00 | 285,579,421.80 | 67.34 |
| 3 | MSD | 947,618,040.93 | 604,057,804.00 | 63.74 |
| 4 | Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida | 733,493,800.00 | 676,767,831.50 | 92.26 |
| 5 | Miradi ya Maendeleo | 7,687,061,273.32 | 4,112,245,896.44 | 53.49 |
| 6 | Mishahara | 18,076,200,388.00 | 14,436,984,500.00 | 79.87 |
| | **Jumla** | **29,229,662,102.25** | **21,145,237,797.87** | **72.34** |

## Mapato; Maelezo kwa vyanzo vya mapato

### A. Mapato ya Ndani

Katika Mwaka wa Fedha **2018 / 2019** Halmashauri ilikadiria kukusanya jumla ya Tshs **1,361,198,600.00**. Mapato haya ni yale yasiyokuwa na masharti. Hadi kufikia mwezi **Juni, 2019** Halmashauri ilikuwa imefanikiwa kukusanya kiasi cha Tshs. **1,029,602,344.13** Sawa na asilimia **75.64**

Kwa upande wa **Mapato yaliyo na masharti**, yaani ada za shule, CHF, NHIF na User fee jumla ya shs**. 424,090,000.00** zilikadiriwa kukusanywa ambapo hadi kufikia mwezi **Juni, 2019** kiasi cha shs. **285,579,421.80** kilikuwa kimekusanywa sawa na asilimia 67.34.

### B. Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida.

Halmashauri ilikadiria kupokea kiasi cha Tshs. **733,493,800.00** kutoka chanzo cha Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida. Chanzo hiki kinajumuisha fedha za Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida na

Fidia kwa vyanzo vilivyofutwa –'GPG'. Halmashauri katika kipindi hicho ilifanikiwa kupokea kiasi cha Tshs. **676,767,831.50** sawa na asilimia **92.26** ambapo kiasi cha Tshs. **659,703,568.20** kiliweza kutumika.

**C. Miradi ya Maendeleo**

Katika Mwaka wa Fedha **2018 /2019** Halmashauri ya Mji Kasulu ilipanga kukusanya na kutumia jumla ya Tshs **7,687,061,273.32** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, fedha hizo zilitegemewa kupokelewa kutoka Serikali Kuu na Wafadhili. Aidha, kiasi cha Tshs. **390,416,000.00** kilitengwa kupitia Mapato ya Ndani kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kwa mwaka wa fedha 2018 / 2019 jumla ya Tshs. **4,310,598,604.96** zimeweza kupokelewa/kukusanywa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo sawa na asilimia 53.4. Fedha hizo zimepokelewa/kukusanywa kutoka katika vyanzo vya Lipa kwa **Matokeo (RBF), TASAF**, **Mfuko wa Jimbo**, **Elimu bila Malipo (Msingi na Sekondari), THPS**, **UNICEF, EQUIP, Mradi wa Ulinzi wa Mtoto (UNICEF), Mradi wa Kuzuia Udumavu (IMA Health), Program ya Usafi wa Mazingira (NSC) na Mapato ya Ndani.**

## Mapokezi ya fedha kwa Bajeti ya nyongeza.

Halmashauri ya mji Kasulu ilipokea fedha kwa bajeti ya nyongeza kwa mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo kiasi cha shilingi **526,044,298.18** kwa ajili ya ujenzi wa meza katika soko la Sofya, Fedha kutoka UNICEF kwa ajili ya mshahara wa mtumishi wa Ustawi wa Jamii, Usajili wa watoto chini ya miaka mitano (U5BR), fedha za **EP4R motisha**, Mradi wa Ujana Salama (Cash Plus), Usafi wa Mazingira na fedha za **miradi ya Maji ya mwaka 2017/2018**. Fedha hizi ni zile zilizopokelewa katika akaunti za Halmashauri.

Taasisi za Halmashauri ya Mji yaani shule na zahanati pia zilipokea fedha kiasi cha Tshs **1,750,344,672.00** kutoka chanzo cha Fedha cha EP4R, Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) na Shirika la UNFPA. Fedha hizi zilikuwa ni kwa ajili ya kuimarisha miundombinu katika shule za Msingi, Sekondari na Zahanati.

**Jedwali 2: Makadirio ya Mapato na Mapokezi halisi ya fedha 2018/2019 kwa miradi ya maendeleo**

| Na | Chanzo cha Fedha | Bajeti Idhinishwa | Mapokezi | % | Matumizi | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mpango wa Kusaidia Kaya Masikini (TASAF). | 1,202,910,000.00 | 642,622,880.00 | 53.4 | 642,622,880.00 | 100 |
| 2 | Mradi wa Maji (NWSSP) | 868,312,000.00 | 10,000,000.00 | 1.15 | 10,000,000.00 | 100 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 3 | Program ya Usafi wa Mazingira | 11,000,000.00 | 11,000,000.00 | 100 | 11,000,000.00 | 100 |
| 4 | Mradi wa Ulinzi wa Mtoto (UNICEF) | 134,407,000.00 | 84,564,000.00 | 62.9 | 84,253,044.20 | 99.63 |
| 5 | Mradi wa elimu ya Ufundi kwa watoto walio nje ya shule (UNICEF) | 78,000,000.00 | 55,722,000.00 | 71.4 | 47,459,500.00 | 85.17 |
| 6 | Jengo la Utawala | 2,300,000,000.00 | 1,000,000,000.00 | 43.5 | 0 | 0 |
| 7 | Mfuko wa Jimbo (CDCF) | 44,190,000.00 | 42,190,000.00 | 95.5 | 39,690,000.00 | 94.1 |
| 8 | Mradi wa Equip | 511,575,000.00 | 288,689,581.00 | 56.4 | 158,233,061.00 | 54.8 |
| 9 | Elimu Msingi Bila Malipo | 664,584,000.00 | 565,130,032.71 | 85.04 | 565,130,032.71 | 100 |
| 10 | Elimu Sekondari Bila Malipo | 453,926,000.00 | 429,932,119.73 | 94.71 | 429,932,119.73 | 100 |
| 11 | Mradi wa Afya Lipa kwa Matokeo (RBF) | 924,984,873.32 | 496,485,183.00 | 53.7 | 371,941,919.00 | 74.9 |
| 12 | Mfuko wa Pamoja wa Afya HSBF | 386,333,000.00 | 405,472,800.00 | 104.95 | 338,185,150.00 | 83.4 |
| 14 | Mradi wa Kuzuia Udumavu IMA HEALTH | 62,210,000.00 | 57,070,000.00 | 91.7 | 52,464,624.66 | 94.07 |
| 15 | Mradi wa Kudhibiti UKIMWI wa THPS | 37,449,400.00 | 16,285,900.00 | 43.49 | 16,213,885.56 | 99.56 |
| 16 | Mradi wa Global Fund | 7,180,000.00 | 7,081,400.00 | 98.6 | 0 | 0 |
| | **Jumla ya Serikali Kuu na Wafadhili** | **7,687,061,273.32** | **4,112,245,896.44** | | **2,767,437,172.66** | **66.4** |
| | Mapato ya Ndani | 390,416,000.00 | 198,352,708.52 | 50.8 | 197,352,708.52 | 99.5 |
| | **JUMLA KUU** | **8,077,477,273.32** | **4,310,598,604.96** | **53.4** | **2,964,789,881.18** | **68.7** |

**FEDHA KWA BAJETI YA NYONGEZA (SUPPLEMENTARY BUDGET) ZILIZOPOKELEWA KWA BAJETI YA NYONGEZA**

**i. Bajeti ya nyongeza katika akaunti za Halmashauri.**

Halmashauri katika kipindi cha Julai – Juni, 2018/ 2019 ilipokea fedha kiasi cha Tshs. **526,044,298.18** ikiwa ni bajeti ya nyongeza kutoka vyanzo mbalimbali kama jedwali hapo chini linavyoonesha.

**Jedwali 3: Fedha zilizopokelewa katika bajeti ya nyongeza kwenye akaunti za Halmashauri.**

| Na | Chanzo cha Fedha | Kiasi cha Fedha Kilichopokelewa | Maelezo |
|---|---|---|---|
| 1 | Mradi wa UNICEF Usajili wa watoto (U5BR) | 67,443,120.00 | Fedha hii ilipokelewa katika akaunti ya miradi na baadae ilirudishwa UNICEF kwa maelekezo yaliyotolewa na UNICEF |
| 2 | Program ya Usafi wa Mazingira | 4,000,000.00 | Fedha hii ilipokelewa kwa ajili ya shughuli za ukusanyaji wa takwimu za wananchi wasiokuwa na vyoo na kusimamia hali ya usafi wa Mji wa Kasulu. Ukusanyaji wa takwimu na usimamizi ulifanyika. |
| 3 | Program ya Usafi wa Mazingira (SWASH)-Elimu Msingi | 6,000,000.00 | TZS 3,000,000 ilipokelewa kwa ajili ya ujenzi wa matundu (4) ya vyoo na chumba maalum kimoja cha wanafunzi wa kike katika shule ya msingi Karunga na TZS 3,000,000 kwa ajili ya shughuli za usimamizi na ufuatiliaji wa hali ya miundombinu ya vyoo mashuleni. Zoezi la usimamizi na ufuatiliaji wa huduma za maji, elimu ya afya na usafi wa mazingira shuleni ulifanyika kwa muda wa siku 10 na watumishi 7 walishiriki zoezi hilo.kazi ya kujenga msingi na |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | kumwaga jamvi la jengo la vyoo ulikamilika. Kazi inayoendelea ni kujenga ukuta. Vifaa vyote vya ujenzi vimenunuliwa. |
| 4 | Mradi wa Ulinzi wa Mtoto (UNICEF) – Fedha za mshahara wa mtumishi | 12,248,208.00 | Fedha ilipokelewa katika kipindi cha kuanzia Julai – Juni 2018/2019 kwa ajili ya malipo ya mshahara kwa mtumishi aliyeajiriwa na shirika la UNICEF. Mtumishi alilipwa stahiki zake. |
| 5 | Usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya EP4R | 16,000,000.00 | Fedha hii ilipokelewa kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya ujenzi wa miundombinu ya madarasa na vyoo katika Shule za Msingi na Sekondari. Usimamizi na ufuatiliaji wa ujenzi wa miundombinu ya shule ulifanyika. |
| 6 | Mradi wa Ujana Salama (CASH PLUS)- TASAF | 28,470,000.00 | Halmashauri ilipokea fedha kwa ajili ya mradi mpya wa 'ujana salama'. Mradi ulitambulishwa kwa Wah. Madiwani na Wakuu wa Idara. Mafunzo kwa 'TOTs' yalitolewa kwa watumishi 10 wa Halmashauri ya Mji Kasulu. Wafundishaji hao 10 waliopewa mafunzo walifanya utambuzi kwa wanufaika. |
| 7 | Fedha za miradi ya maji ya mwaka 2017/2018 | 148,756,591.00 | Katika kipindi cha Julai – Juni, 2018/2019 Halmashauri ilipokea fedha kiasi cha shs. 148,756,591.00 kwa ajili ya miradi ya mwaka wa fedha 2017/2018 ambazo zililipwa kwa kazi ambazo zilitekelezwa. |
| 8 | Fedha za Motisha (EP4R) kwa Sekta ya Elimu | 194,044,343.98 | Halmashauri ilipokea na kutumia fedha za motisha mfuko wa EP4R kwa kazi za upangaji wa IKAMA ya walimu, ukusanyaji wa takwimu, ufuatiliaji na tathmini kwa shule za Msingi na Sekondari. Kazi hizo zilikamilika. |
| 9 | Ujenzi wa meza katika soko la Sofya | 49,082,035.20 | Meza 35 (sawa na 70 kwa moja moja) zilijengwa katika soko la sofya. Kazi zilizofanyika ni uchimbaji wa msingi na ujenzi, |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | ujazaji kifusi na usindiliaji, upangaji wa mawe kwa ajili ya 'hard core' umwagaji wa jamvi na ujenzi wa meza. Ujenzi wa meza 70 ulikamilika. |
| | **JUMLA** | **526,044,298.18.00** | |

**ii. Fedha zilizopokelewa katika Akaunti za Shule**

Halmashauri katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai hadi Juni 2018/2019 ilipokea fedha katika taasisi zake (shule na zahanati) kiasi cha Shilingi **1,750,344,672.00 kwa mchanganuo ufuatao:-**

- Kiasi cha Shilingi 778,130,000 kilipokelewa kupitia chanzo cha EP4R kwa ajili ya miundombinu ya shule za sekondari
- Kiasi cha Shilingi 255,700,000.00 kilipokelewa kupitia chanzo cha EP4R kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji miundombinu ya shule za Msingi
- Kiasi cha Shilingi 305,500,000.00 kilipokelewa kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) kwa ajili ya ujenzi na ukamilishaji wa miundombinu katika shule za msingi na sekondari.
- Kiasi cha Shilingi 286,014,672.00 kilipokelewa katika zahanati za Ruhita, Mwanga na Mwibuye kwa ajili ya ujenzi wa ‘Maternity Wing’ wa vituo hivyo, fedha kutoka Shirika la **UNFPA.**

**Jedwali 4: Mchanganuo wa fedha hizo na hatua ya utekelezaji wa miradi ni kama inavyooneshwa hapo chini:-**

| **Na.** | **Chanzo cha fedha / Mradi** | **Kiasi cha Fedha Kilichopokelewa** | **Maelezo** |
|---|---|---|---|
| 1 | Mradi wa ujenzi wa bweni na bwalo katika shule ya sekondari ya Kasange | 95,500,000.00 | Fedha ilipokelewa kwenye akaunti ya shule kwa ajili ya ujenzi wa bweni na bwalo kutoka Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA). Ujenzi wa Bweni ulikamilika na jengo linatumika na ujenzi wa Bwalo umefikia hatua ya ukamilishaji (uwekaji vigae) |
| 2 | Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa shule ya msingi Kibagwe | 60,000,000.00 | Fedha ilipokelewa kwenye akaunti ya shule kutoka mfuko wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa shule ya |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | msingi Kibagwe. Ujenzi ulikamilika |
| | Ujenzi wa mabweni katika shule ya sekondari ya Muhunga | 150,000,000.00 | Fedha zimepokelewa katika shule ya sekondari Muhunga kutoka Malmlaka ya Elimu Tanzania (TEA) kwa ajili ya ujenzi wa bweni.Mradi umefikia hatua ya ujenzi wa lenta. |
| 3 | Shule ya Sekondari Kigoma Grand | 380,730,000.00 | Fedha hii ilipokelewa kutoka chanzo cha Fedha EP4R kwa ajili ya uimarishaji miundombinu kwa shule mpya ya Kigoma Grand. Kazi ilifanyika na shule tayari inatoa huduma. |
| 4 | Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa shule ya Sekondari Bogwe | 60,000,000.00 | Fedha imepokelewa kwenye akaunti ya shule kutoka chanzo cha Fedha EP4R kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa shule ya sekondari Bogwe. Ujenzi wa Vyumba vitatu vya madarasa ulikamilika. |
| 5 | Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa na matundu 6 ya vyoo shule ya sekondari Kigodya | 66,600,000.00 | Fedha ilipokelewa kwenye akaunti ya shule kutoka chanzo cha Fedha EP4R kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo shule ya sekondari Kigodya. Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa na vyoo Ulikamilika |
| 6 | Ujenzi wa madarasa 2 na matundu 6 ya vyoo shule ya Msingi Nyansha. | 46,600,000.00 | Fedha imepokelewa kwenye akaunti ya shule kutoka chanzo cha EP4R kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo shule ya msingi Nyansha. Ujennzi wa madarasa 2 na matundu 6 ya vyoo ulikamilika |
| 7 | Ujenzi wa madarasa 3 na matundu 6 ya vyoo shule ya sekondari Kinkati. | 66,600,000.00 | Fedha imepokelewa kwenye akaunti ya shule kutoka chanzo cha Fedha EP4R kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo shule ya sekondari Kinkati. Ujenzi wa Madarasa 3 na matundu 6 ya vyoo ulikamilika |
| 8 | Ujenzi wa madarasa 3 na matundu 6 ya vyoo shule ya sekondari Nyantare. | 66,600,000.00 | Fedha imepokelewa kwenye akaunti ya shule kutoka chanzo cha Fedha EP4R kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo ambao Ujenzi ulikamilika. |
| 9 | Ujenzi wa madarasa 3 na matundu 10 ya vyoo shule ya sekondari Ruhita. | 71,000,000.00 | Fedha imepokelewa kwenye akaunti ya shule kutoka chanzo cha Fedha EP4R kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo shule ya sekondari Ruhita. Ujenzi wa madarasa 3 na matundu 10 ya vyoo ulikamilika. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 10 | Ujenzi wa madarasa 3 na matundu 6 ya vyoo shule ya sekondari Mwibuye. | 66,600,000.00 | Fedha imepokelewa kwenye akaunti ya shule kutoka chanzo cha Fedha EP4R kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa na matundu ya vyoo shule ya sekondari Mwibuye. Ujenzi wa madarasa 3 na vyoo matundu 6 Ulikamilika. |
| 11 | Ujenzi wa madarasa 2 na matundu 6 ya vyoo shule ya Msingi Kasyenene. | 46,600,000.00 | Fedha imepokelewa kwenye akaunti ya shule kutoka chanzo cha Fedha EP4R kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa .Ujenzi wa madarasa 2 na matundu ya vyoo 6 ulikamilika. |
| 12 | Ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa Mubondo Sekondari | 25,000,000.00 | Fedha imepokelewa kwenye akaunti ya shule kutoka Serikali Kuu (chanzo cha Central Government Other Source). Ujenzi wa madarasa 2 ulikamilika. |
| 13 | Ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa Kigodya Sekondari | 25,000,000.00 | Fedha ilipokelewa kwenye akaunti ya shule kutoka Serikali Kuu (chanzo cha Central Government Other Source). Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa Ulikamilika. |
| 14 | Ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa Nyumbigwa Sekondari | 25,000,000.00 | Fedha ilipokelewa kwenye akaunti ya shule kutoka Serikali Kuu (chanzo cha Central Government Other Source). Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa ulikamilika. |
| 15 | Ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa Kinkati Sekondari | 25,000,000.00 | Fedha ilipokelewa kwenye akaunti ya shule kutoka Serikali Kuu (chanzo cha Central Government Other Source). Ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa ulikamilika. |
| 16 | Ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba 5 vya madarasa Hwazi Sekondari | 25,000,000.00 | Fedha ilipokelewa kwenye akaunti ya shule kutoka Serikali Kuu (chanzo cha Central Government Other Source). Ukamilishaji wa Ujenzi wa vymba 5 vya madarasa ulikamilika. |
| 17 | Ukamilishaji wa ujenzi wa chumba 1 cha darasa Shule ya Msingi Juhudi | 12,500,000.00 | Fedha ilipokelewa kwenye akaunti ya shule kutoka chanzo cha Fedha P4R kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa chumba 1 cha darasa. Mradi ulikamilika. |
| 18 | Ukamilishaji wa ujenzi wa chumba 1 cha darasa Shule ya Msingi | 12,500,000.00 | Fedha ilipokelewa kwenye akaunti ya shule kutoka chanzo cha Fedha P4R kwa ajili ya ukamilishaji wa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Junga | | ujenzi wa chumba 1 cha darasa. Mradi ulikamilika. |
| 19 | Ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba 2 vya darasa Shule ya Msingi Kasulu | 25,000,000.00 | Fedha ilipokelewa kwenye akaunti ya shule kutoka chanzo cha Fedha EP4R kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa. Vyumba viwili vilikamilika. |
| 20 | Ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba 2 vya darasa Shule ya Msingi Mugandazi | 25,000,000.00 | Fedha ilipokelewa kwenye akaunti ya shule kutoka chanzo cha Fedha EP4R kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa. Ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa ulikamilika. |
| 21 | Ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba 2 vya darasa Shule ya Msingi Nyabuyange | 25,000,000.00 | Fedha ilipokelewa Fedha EP4R kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa. Mradi Ulikamilika. |
| 22 | Ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba 2 vya darasa Shule ya Msingi Uhuru | 25,000,000.00 | Fedha ilipokelewa kwenye akaunti ya shule kutoka chanzo cha Fedha EP4R kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba 2 vya madarasa. Mradi ulikamilika. |
| 23 | Ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba 3 vya darasa Shule ya Msingi Nyangwa | 37,500,000.00 | Fedha ilipokelewa kwenye akaunti ya shule kutoka chanzo cha Fedha EP4R kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa vyumba 3 vya madarasa. Mradi ulikamilika. |
| 24 | Ujenzi/ukarabati wa wodi ya wazazi zahanati ya Mwibuye | 95,338,224.00 | Fedha ilipokelewa tarehe 15.06.2019 kwenye akaunti ya zahanati kutoka Shirika la UNFPA kwa ajili ya ujenzi/ukarabati wa wodi ya wazazi. Kazi ya ujenzi itafanyika katika mwaka wa fedha 2019/2020. |
| 25 | Ujenzi/ukarabati wa wodi ya wazazi zahanati ya Ruhita | 95,338,224.00 | Fedha ilipokelewa tarehe 15.06.2019 kwenye akaunti ya zahanati kutoka Shirika la UNFPA kwa ajili ya ujenzi/ukarabati wa wodi ya wazazi. Kazi ya ujenzi itafanyika katika mwaka wa fedha 2019/2020. |
| 26 | Ujenzi/ukarabati wa wodi ya wazazi zahanati ya Mwanga | 95,338,224.00 | Fedha ilipokelewa tarehe 15.06.2019 kwenye akaunti ya zahanati kutoka Shirika la UNFPA kwa ajili ya ujenzi/ukarabati wa wodi ya wazazi. Kazi ya ujenzi itafanyika katika mwaka wa fedha 2019/2020. |
| | **JUMLA** | **1,750,344,672.00** | |

****Vyumba vipya vya madarasa vilivyojengwa kwa chanzo cha fedha za EP4R vimeongezewa na ofisi ya walimu katikati ya vyumba hivyo ili kusaidia ofisi za walimu ingawa haikulengwa katika mpango wa awali.

**Matumizi**

Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Halmashauri ilipanga kukusanya na kutumia kiasi cha Tshs. **29,229,662,102.25** kutoka katika vyanzo mbalimbali, hadi kufikia mwezi Juni, 2019 jumla ya Tshs**. 21,145,237,797.87** ziliweza kupokelewa. Katika kipindi hicho pia Halmashauri iliweza kutumia fedha kiasi cha Tshs. **19,606,779,220.24** kutoka katika fedha iliyopokelewa.

**Jedwali 5. Matumizi ya Fedha kwa mwaka 2018/2019**

| Na | Chanzo cha fedha | Bajeti Idhinishwa | Mapokezi | % | Matumizi | % |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Ndani | | | | | |
| i. | Mapato ya Ndani yasiyo na Masharti | 1,361,198,600.0 | 1,029,602,344.13 | 75.64 | 919,868,231.91 | 89.34 |
| ii. | Mapato ya Ndani yenye Masharti | 424,090,000.00 | 285,579,421.80 | 67.34 | 248,290,785.47 | 86.94 |
| 2 | MSD | 947,618,040.93 | 604,057,804.00 | 63.74 | 574,494,962.00 | 95 |
| 3 | Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida | 733,493,800.00 | 676,767,831.50 | 92.26 | 659,703,568.20 | 97.47 |
| | Miradi ya Maendeleo | 7,687,061,273.32 | 4,112,245,896.44 | 53.49 | 2,767,437,172.66 | 67 |
| 4 | Mishahara | 18,076,200,388.00 | 14,436,984,500.00 | 79.87 | 14,436,984,500.00 | 100 |
| | Jumla | 29,229,662,102.25 | 21,145,237,797.87 | 72.34 | 19,606,779,220.24 | 92.95 |

**Mafanikio katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2018/2019**

Halmashauri ya Mji wa Kasulu ilipata mafanikio kadhaa kwa bajeti ya mwaka 2018/2019, baadhi yake ni kama ifuatavyo;-

Utawala

- Halmashauri ya Mji imeendelea na **ujenzi wa jengo la Ofisi za Halmashauri** na katika Mwaka huo wa fedha Halmashauri ilifanikiwa kupokea kiasi cha Tshs 1,000,000,000.00 sawa na asilimia 43.5 kati ya Tshs. 2,300,000,000.00 zilizokasimiwa. Hali hii iliendelea kutoa matumaini kwa watumishi wa Halmashauri ya Mji kupata mazingira mazuri ya kufanyia kazi kwa wakati/ mapema.
- Halmashauri imeweza kusimamia kufanyika kwa vikao vya kisheria ngazi ya halmashauri kama inavyotakiwa kwa mujibu wa taratibu na sheria.

- Halmashauri ilifanikiwa kupokea **watumishi wapya (ajira mpya) 74**. Watumishi hao walikuwa ni kwa idara za Elimu Msingi 23, Elimu Sekondari 9, Afya 34 na Utawala watumishi 8.
- Jumla ya watumishi 537 walikidhi vigezo vya kupanda vyeo kwa ikama ya mwaka 2017/2018. Watumishi 447 kati ya hao ni wa Elimu Msingi na 90 ni Elimu Sekondari. Tayari walimu 509 wameshabadilishiwa mishahara yao na walimu 28 bado hawajabadilishiwa. Halmashauri inaendelea kuwasiliana na Wizara ili watumishi wote waweze kubadilishiwa mishahara.
- Jumla ya watumishi 40 wa Idara nyingine walikidhi vigezo vya kupanda vyeo. Watumishi 18 kati ya hao tayari wamebadilishiwa mishahara yao na wengine waliobaki wanasubiri 'approval'. Halmashauri inaendelea kuwasiliana na Wizara ili watumishi wote waweze kubadilishiwa mishahara
- Jumla ya watumishi 9 wa Idara nyingine walikidhi vigezo vya kubadilishiwa miundo. Watumishi watano (5) kati ya hao wameweza kubadilishiwa miundo. Watumishi waliosalia wanasubili 'approval'. Halmashauri inaendelea kuwasiliana na Wizara ili watumishi wote waweze kubadilishiwa miundo yao.

- **Uboreshaji wa huduma za afya.**
  Halmashauri imefanikiwa kupanua huduma zinazotolewa Hospitali ya Mji Kasulu. Katika kipindi hicho, Halmashauri imefanikiwa kujenga **Theatre**, **wodi na jengo la mionzi**. Majengo haya tayari yanatumika na kutoa huduma kwa wananchi na hivyo huduma imepanuliwa katika Hospital Halmashauri kwa ujumla.
    - ✓ *Jengo la upasuaji linategemewa kuongeza ufanisi wa kutoa huduma mbalimbali za upasuaji kwani kuna vyumba bora viwili vya upasuaji tofauti na kimoja kilicho kuwepo awali hivyo kupunguza vifo na madhara yatokanayo na magonjwa ya upasuaji.*
    - ✓ *Jengo la mionzi linategemewa kuwezesha wagonjwa wanaohitaji huduma ya mionzi kupata huduma stahiki kwa wakati na ufanisi. Hivyo kuondoa usumbufu wa wagonjwa kufuata huduma katika hospitali ya Kabanga na ile ya Maweni .*
    - ✓ *Jengo la wodi linategemewa kuwezesha wanawake wenye magonjwa ya via vya uzazi na wajawazito wenye matatizo ya mimba chini ya wiki 28 kupata huduma bora hivyo kupunguza msongamano katika wodi ya wanawake wenye magojwa ya upasuaji walipokuwa wakichangamana*

- Halmashauri kwa kushirikiana na jamii inaendelea na ujenzi wa zahanati ya Marumba. Wananchi wameendelea kutoa michango yao ya fedha na nguvu kazi na kwa upande wa Halmashauri imeendelea kutoa fedha kadiri inavyopatikana ili kuweza kukamilisha mradi huo. Na tayari Halmashauri imeshapokea kiasi cha shilingi 100,000,000.00 kwa ajili ya umaliziaji wa zahanati hiyo kutoka serikali kuu.

- Katika sekta ya Elimu Msingi, Halmashauri ilifanikiwa kujenga vyumba vya madarasa 20, matundu 12 ya vyoo na kukamilisha maboma 13 ya madarasa katika shule za msingi kwa wastani jumla ya wanafunzi 800 wameboreshewa mazingira ya kujifunzia na hivyo kuendelea kupunguza ukubwa wa tatizo la msongamano wa watoto shuleni.

- Hali ya ufaulu darasa la saba iliongezeka kutoka alilimia 67 mwaka 2018 hadi kufikia asilimia 70.25 mwaka 2019,Watoto wote waliofaulu walipata nafasi ya kujiunga kidato cha kwanza.

- Kwa upande wa elimu ya sekondari, Halmashauri ilifanikiwa kujenga na Kukamilisha vyumba 32 vya madarasa, matundu 34 ya vyoo .Halmshauri pia ilifanikiwa kukamilisha bweni moja katika shule ya sekondari kasange na inaendelea kukamilisha Bweni katika shule ya sekondari Muhunga hali ambayo inategemewa kuongeza ufaulu kwa wanafunzi hasa wa kike kwa kuwa watapata muda mwingi wa kujisomea na kupunguza vishawishi vinavyoweza kuathiri umakini wao katika masomo.
- Hali ya ufaulu kwa kidato cha nne imeongezeka kutoka asilimia 85 mwaka 2018 hadi kufikia asilimia 86 mwaka 2019
- Halmashauri ilifanikiwa kupanua mradi wa maji wa Heru Juu, na kuweza kuhudumia maeneo ya karunga, shule ya sekondari Kasange na na mtaa wa Kasange.

**Changamoto**

Katika kutekeleza bajeti ya Mwaka wa Fedha 2018/2019 Halmashauri ilikabiliwa na changamoto kadhaa kama inavyooneshwa hapo chini.

i. Fedha za miradi ya maendeleo hazikupokelewa kama ilivyokuwa imepangwa, na baadhi ya fedha zilizopokelewa hazikufika kwa wakati (kulingana na mpango kazi).

ii. Hospitali ya Mji Kasulu inahudumia watu wengi, ikiwa ni wale wa kutoka katika Halmashauri ya Mji, Halmashauri za Wilaya za Kasulu, Buhigwe, Uvinza na sehemu ya Halmashauri ya Kigoma. Licha ya kuhudumia eneo kubwa hivyo bado bajeti yake ni ndogo ikilinganishwa na mahitaji.

iii. Hospitali ya wilaya pia hupokea wagonjwa wengi wa Msamaha hivyo kuathiri mapato.

iv. Ukomo wa Bajeti yaani (Ceiling) kutobalilika kwani Stahiki nyingi za watumishi hazilipwi kwa wakati kutokana na uchache huo wa rasilimali.

v. Halmashauri iliendelea kuwa na changamoto ya upungufu wa watumishi katika kada mbalimbali. Hali hiyo imekuwa inapelekea watumishi waliopo kutumia muda wa ziada kutekeleza majukumu yao ili kufikia matokeo yanayostahili. Inategemewa kuwa kukiwa na watumishi wa kutosha, kila mmoja atakuwa na nafasi ya kutekeleza majukumu yake kulingana na ratiba, hivyo, kuongeza ufanisi.

vi. Miundombinu ya kutolea huduma bado ni michache na mingine ni chakavu hali ambayo inachangia kupelekea mazingira duni ya utoaji na upokeaji huduma. Mahitaji ya vyumba vya madarasa, nyumba za walimu, vyumba vya maabara n.k
vii. Ufinyu wa bajeti umekuwa unapelekea uwezo wa Halmashauari kuwa mdogo kuweza kutatua changamoto za jamii kwa wakati, hivyo, jamii inatakiwa kusubili kwa wakati hadi pale rasilimali zinapopatikana.
viii. Mafanikio ya uuzaji wa vitambulisho vya wajasilia mali pia yamepelekea kupungua kwa makusanyo ya Halmashauri.
ix. Upungufu wa watumishi Halmashauri ina upungufu wa watumishi 862. Mahitaji ni watumishi 2332. Mpaka sasa tuna watumishi 1470.

**Mkakati.**

i. Halmashauri imepanga kuendelea kuimarisha mapato yake ya ndani kadiri itakavyowezekana kwa kuibua na kuanzisha vyanzo vipya kama ifuatavyo.
- Ujenzi wa vibanda eneo la kumsenga
- Kujenga vibanda vya biashara eneo la Nyachijima kata ya Kigondo.
- Kodi ya huduma katika kiwanda cha nguzo kilichoanzishwa kata ya Heru Juu

ii. Kuendelea kuomba Wizara husika kuiongozea bajeti Halmashauri ili iweze kuboresha huduma kwa wananchi wengi na kwa wakati.
iii. Kuendelea kuziomba Wizara kutoa fedha kwa wakati na kulingana na bajeti iliyoidhinishwa

iv. Halmashauri ya Mji inaendelea kuwasihi wananchi kuendelea kuchangia shughuli za maendeleo kama ambavyo wamekuwa wakiteleza hilo katika miradi mbalimbali.

v. Kuendelea kutenga nafasi wazi za ajira katika bajeti ili kuweza kupunguza changamoto ya upungufu wa watumishi.

vi. Kuendelea kufuatilia kwa karibu watumishi kupandishwa vyeo, kubadilishiwa miundo yao ili kuleta ufanisi katika utendaji wao.

## 2.2. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2019/2020, KUFIKIA DESEMBA, 2019

Katika Mwaka wa Fedha 2019/ 2020 Halmashauri ya Mji ilikadiria kukusanya kiasi cha Tshs. 30,298,587,813.27 kutoka vyanzo mbalimbali. Vyanzo hivyo ni Mapato ya Ndani yasiyo na masharti 1,362,500,000.00. Mapato ya Ndani yenye masharti Tshs. 480,306,000.00, Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida Tshs. 1,294,234,540.00, fedha za Miradi ya Maendeleo Tshs. 6,241,205,323.27, MSD Tshs. 294,814,978.41 na Mishahara Tshs. 20,920,341,950.00.

**Mapato**

Katika kipindi hicho cha Julai – Desemba, 2019 Halmashauri imeweza kukusanya/ kupokea kiasi cha Tshs. 8,407,900,898.79 sawa na asilimia 26.26 kama jedwali hapo chini linavyoonesha.

**Jedwali 6: Makisio ya Mapato na Mapato halisi kwa kipindi cha Julai – Desemba, 2019**

| Na | Chanzo cha Fedha | Makisio | Mapato Halisi | Asilimia |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Ndani yasiyo ya masharti | 1,362,500,000.00 | 601,064,046.74 | 44.1 |
| 2 | Mapato ya Ndani yenye Masharti | 480,306,000.00 | 121,222,368.78 | 25.24 |
| 3 | MSD | 947,618,041.93 | 74,939,300.00 | 7.9 |
| | Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida | 1,294,234,540.00 | 682,733,740.00 | 52.75 |
| 4 | Miradi ya Maendeleo | 5,293,587,282.00 | 580,540,176.96 | 10.97 |
| 5 | Mishahara | 20,920,341,950.00 | 6,048,342,252.66 | 28.91 |
| | **Jumla** | **30,298,587,813.27** | **8,407,900,898.79** | **26.26** |

### A. Mapato ya Ndani Yasiyo na Masharti

Kama inavyooneshwa kwenye jedwali hapo juu, katika Mwaka wa Fedha 2019/ 2020 jumla ya Tshs. 1,362,500,000.00 zilikadiriwa kukusanywa kupitia chanzo hiki cha Mapato ya Ndani. Hadi kufikia mwezi Desemba, 2019 jumla ya Tshs. 601,064,046.74sawa na asilimia 44.1 zimeweza kukusanywa.

Halmashauri imekumbana na changamoto katika ukusanyaji wa mapato katika kipindi hiki, baadhi ya Changamoto ambazo zilizojitokeza ni kama ifuatavyo:-

i. Halmashauri bado haijafanikiwa kujenga vibanda katika eneo la Kumsenga kutokana na upungufu wa fedha. Makadirio ya Mwaka wa fedha 2019/2020 yalihusisha pia vibanda vya Kumsenga, hivyo, mapato yaliyokusudiwa kukusanywa kupitia chanzo hiki 144,000,000.00 bado hayajaanza kupatikana na hivyo kuathiri makusanyo.

ii. Makadirio ya mapato pia yalihusisha uuzaji wa viwanja, chanzo hiki hakikuweza kutoa mapato yeyote, viwanja havijanunuliwa katika kipindi hiki.

iii. Mafanikio ya uuzaji wa vitambulisho vya wajasilia mali pia yamepelekea kupungua kwa makusanyo ya Halmashauri.

Hizo ni baadhi ya **changamoto** ambazo zimejitokeza katika ukusanyaji wa mapato ya Ndani kwa kipindi cha Julai – Desemba, 2019

Kuna baadhi ya vyanzo ambavyo Halmashauri imeweza **kuvuka lengo** kwa makusanyo, mfano ni chanzo cha **ushuru wa mazao ya maharagwe**, tayari makusanyo yamefika asilimia **115.2**, chanzo cha **ushuru wa mazao mengine ya chakula** ambacho kimefikia asilimia **290.2, Ushuru wa mahindi 133.6 na Ushuru wa mifugo umefikia asilimia 120.6**

Baadhi ya vyanzo pia makusanyo yameweza **kuvuka asilimia 50** katika kipindi cha nusu mwaka, vyanzo hivyo ni **ushuru wa mchele asilimia 93.8, Ada na ukaguzi wa upimaji wa viwanja ambao makuanyo yake yamefikia asilimia 81.9. Vibali vya Ujenzi** ambao makusanyo yake yamefikia **asilimia 88.9** na **Ada ya leseni za biashara 74.7%**

Lengo la Halmashauri ni kuhakikisha inafanya vizuri katika makusanyo yake ya ndani kwani ndicho chanzo cha kuaminika katika utoaji wa huduma kwa wananchi. Katika kipindi cha mwaka wa fedha kilichobaki, usimamizi kwa vyanzo vyote vya mapato utaongezwa na kuweka msukumo wa kutosha katika vyanzo vinavyoonekana kutokuwa na mwenendo mzuri ili kuhakikisha mapato yaliyokusudiwa yanakusanywa ili kuweza kupanua uwezo wa kuhudumia wananchi.

**Mapato ya Ndani yenye masharti**

Kwa upande wa mapato yaliyo na masharti, yaani ada za shule, CHF, NHIF na User fee jumla ya Tshs. **480,306,000.00** zilikadiriwa kukusanywa na hadi kufikia mwezi Desemba, 2019 kiasi cha Tshs. **121,222,368.78** kimeweza kimekusanywa sawa na **asilimia 25.24.**

**Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida**.

Halmashauri ilikadiria kupokea kiasi cha Tshs. **1,294,234,540.00** kutoka chanzo cha Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida. Chanzo hiki kinajumuisha fedha za Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida na Fidia kwa vyanzo vilivyofutwa –'GPG', hadi kufikia mwezi Desemba, 2019 jumla ya **Tshs 659,564,740.00** zilikuwa zimepokelewa sawa na asilimia 69 kama jedwali hapo chini linavyoonesha.

| Na | Chanzo cha Fedha | Bajeti Idhinishwa | Mapokezi | % |
|---|---|---|---|---|
| i. | Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida | 1,242,873,540.00 | 669,513,740.00 | 53.86 |
| ii. | Fidia kwa vyanzo vilivyofutwa | 51,361,000.00 | 13,240,000.00 | 25.78 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | **Jumla** | **1,294,234,540** | **682,753,740.00** | **79.64** |

**Mishahara.**

Katika Mwaka wa Fedha **2019/2020** Halmashauri ilipanga kulipa kiasi cha Tshs. **20,920,341,950.00** Kama mishahara kwa watumishi wake. Kwa kipindi kinachoishia Desemba, 2019 Halmashauri imeweza kulipa mishahara kiasi cha Tshs. **7,314,235,752.60** sawa na asilimia **34.96** ya makisio yote kupitia fungu la 74E4 la Halmashauri ya Mji Kasulu.

**Miradi ya Maendeleo.**

- Katika Mwaka wa Fedha **2019 /2020** Halmashauri ya Mji Kasulu ilipanga kukusanya na kutumia jumla ya Tshs **5,840,585,842.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, fedha hizo zilitegemewa kupokelewa kutoka Serikali Kuu na Wafadhili. Katika mwaka huo pia, kiasi cha Tshs. **546,998,560.00** kilitengwa kupitia Mapato ya Ndani kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia mwezi Desemba, 2019 jumla ya Tshs.767,685,520.96 zimeweza kupokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo sawa na asilimia 16 ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi na kiasi cha Tshs**.** **642,646,532.96** zimeweza kutumika sawa na asilimia 68.6 ya fedha pokelewa.

- Fedha kwa **bajeti ya Nyongeza,** Halmashauri hadi **Desemba, 2019** imeweza kupokea kiasi cha Tshs. **609,800,435.4** kutoka katika vyanzo vya EP4R (Education pay for result), Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), UNICEF, ITC na IMA. Kati ya fedha hizo kiasi cha Shilingi **15,585,354.4** zimepokelewa katika akaunti ya Halmashauri kwa ajili ya ujenzi wa meza katika soko la Sofya Shilingi 12,123,302.4, kulipa mshahara wa Afisa Ustawi wa Jamii shilingi 3,062,052.00 na Kuzuia udumavu kwa watoto wenye chini ya miaka mitano Shilingi 400,000 na Shilingi 594,215,081.00 zilipokelewa kwenye shule ya Msingi Juhudi na shule ya Sekondari Kigoma Grand

**Muhtasari wa miradi inayoendelea kutekelezwa Mwaka wa fedha 2019/2020**

Halmashauri inaendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika mwaka wa fedha **2019/2020**. Muhtasari wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo-

**Ujenzi wa jengo la Utawala katika Halmashauri ya Mji Kasulu.**

Mradi wa ujenzi wa jengo la utawala la Halmashauri ya Mji Kasulu utagharimu kiasi cha Tshs. 4,553,832,910.18 hadi kukamilika. Mradi unaendelea kutekelezwa na Mkandarasi ambaye ni Wakala wa Majengo Tanzania (TBA). Tayari Tshs. 3,000,000,000 zimeshapokelewa katika kipindi cha kuanzia 2016/2017 hadi Juni, 2018/2019. Ujenzi unaendelea.

**Ujenzi wa Meza katika Soko la Sofya.**

Ujenzi huu umefadhiliwa na KIGOMA JOINT PROGRAME (KJP) chini ya Shirika la International Trading Centre (ITC). Halmashauri imeshapokea jumla ya kiasi cha shilingi 61,205,337.60 ambazo zimetumika kujenga meza 55 (za 2 kwa 1) ambazo zinaweza kunufaisha watu 110 kwa pamoja. Halmashauri imeshawasilisha maombi ya fedha kwa ajili utekelezaji mradi huo kwa awamu ya pili . Maombi hayo yameshaidhinishwa na fedha inatarajiwa kupokelewa mwezi januari 2020 ili kuendelea na ujenzi

Halmashauri pia inaendelea na matengenezo ya barabara katika kata za Heru juu, Nyansha, Kimobwa, Kumsenga, Murubona na Murufiti kupitia Mfuko wa Jimbo.

**Miradi ya Elimu Msingi**.

- Ujenzi wa madarasa 3 Shule ya Msingi Juhudi kwa gharama ya shilingi 60,000,000 chanzo cha fedha ni Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA). Ujenzi uko hatua ya upauaji
- Shule ya Msingi Junga ilipokea kiasi cha Tshs 25,093,503/= Mwishoni mwa Mwaka 2018/2019 kwa ajili ya umaliziaji wa ujenzi wa vyumba viwili vya madarasa kutoka chanzo cha fedha EQUIP. Ujenzi uko hatua umaliziaji.

  Ujenzi wa madarasa 2 na matundu 2 ya vyoo vya walimu shule ya Msingi Mwilamvya unatekelezwa kwa kutumia wananchi ambao wamechangia fedha shilingi 11,210,000.00 na matofali, Mfuko wa Jimbo Tshs. 1,000,000.00 na wadau wa kielimu (Bw. Dalili Mausen aliyechangia mifuko 50 ya saruji), Pia Halmashauri ya mji Kasulu ilichangia Mabati 143. Ujenzi uko hatua ya kumalizia ukuta.
- Ukarabati wa chumba kimoja cha darasa na ofisi ya walimu Shule ya Msingi Kimobwa kwa kutumia michango ya wananchi, fedha ya IGA (Income Generation Activities), Mfuko wa Jimbo na Mapato ya Ndani ya Halmashauri ya Mji Kasulu. Ukarabati umefikia hatua ya kupaka rangi.
- Jumla ya shilingi 75,000,000 zimepokelewa katika shule za Msingi Murufiti, Mwibuye na Tulieni kwa kila shule shilingi 25,000,000.00. Matumizi ya pesa hiyo ni kwa ajili ya ukamilishaji wa nyumba za walimu

**Miradi inayotekelezwa katika Elimu Sekondari**

- Ujenzi wa bweni la wasichana Muhunga sekondari kwa gharama ya Tshs. 150,000,000 kwa kutumia Chanzo cha Fedha TEA. Ujenzi wa mradi huu umefikia hatua ya ukamilishaji.

- Ujenzi wa Bwalo dogo la Chakula Shule ya sekondari Kasange kwa gharama ya Tshs. 32,396,000 kwa fedha zilizobaki kwenye ujenzi wa bweni 192,000,000 chanzo cha fedha TEA. Ujenzi wa mradi huu umefikia hatua ya ukamilishaji.

- Ukamilishaji wa jengo la utawala na ujenzi wa miundombinu ya Maji katika shule ya sekondari ya Kigoma Grand kwa gharama ya Tshs. 534,215,081 kwa kutumia chanzo cha fedha EP4R. Kazi zimnaendelea.

**Miradi inayotekelezwa katika Idara ya Afya**

Katika kipindi cha mwezi Julai-Desemba 2019, Idara ya Afya imeweza kutekeleza miradi ifuatayo:

1. Ujenzi wa majengo matatu ya kujifungulia katika Zahanati za Mwanga, Ruhita na Mwibuye (moja katika kila zahanati). Ujenzi huu unatekelezwa kwa fedha kiasi cha Tshs. 288,158,632.00 zilizopokelewa kutoka UNFPA. Ujenzi umefikia hatua ya upauaji.

2. Ujenzi wa uzio wa Hospitali unaojengwa kwa awamu kupitia fedha za Mpango wa Malipo kwa Ufanisi (RBF). Ujenzi wa uzio umefikia asilimia 65 na ujenzi kwa sasa umesimama kutokana na kuisha kwa fedha. Halmashauri itaendelea na ujenzi huu baada ya kupokea fedha kutoka Wizarani.
3. Ujenzi wa Zahanati ya Marumba, ambapo kazi ya uezekaji wa Majengo imekamilika. Tayari kiasi cha Tshs. 100,000,000.00 (Milioni mia moja) kimepokelewa kutoka OR - TAMISEMI kwa ajili ya kumalizia ujenzi huo.

## 2.4. MAPENDEKEZO YA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

Katika Mwaka wa Fedha **2020/2021** Halmashauri ya Mji imekadiria kuwa na bajeti yenye jumla ya Tshs**.** **31,498,339,320.25** kutokana na vyanzo mbalimbali kama inavyooneshwa katika jedwali hapo chini: -

**Jedwali 7; Makadirio ya mapato na Matumizi kwa Mwaka wa fedha 2020/2021**

| Na | Chanzo cha Fedha | Kiasi kinachoombwa |
|---|---|---|
| 1 | Mapato ya Ndani | |
| i | Mapato ya Ndani yasiyo na masharti | 1,475,372,900.00 |
| ii | Mapato ya Ndani yenye masharti | |
| | Ada za shule | 80,456,000.00 |
| | CHF, NHIF, Papo kwa Papo | 344,000,000.00 |
| 2 | Mapato ya shule | 8,750,000.00 |
| 3 | MSD | 947,618,040.93 |
| 4 | Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida | 1,048,549,800.00 |
| 5 | Mishahara | 21,840,096,000.00 |
| 6 | Miradi ya Maendeleo | 5,753,496,579.32 |
| | Jumla | **31,498,339,320.25** |

**Mapato ya Ndani**

**i. Mapato ya Ndani yasiyo ya Masharti.**

Katika Mwaka wa Fedha **2020/2021** Halmashauri ya Mji Kasulu imekadiria kukusanya kiasi cha Tshs. **1,475,372,900.00** kutoka katika vyanzo vyake. Mchanganuo wa maoteo ya makusanyo hayo ni kama inavyooneshwa hapo chini.

**Jedwali 8; Mwenendo wa Mapato ya Ndani mwaka**

| NA | Maelezo ya kifungu | Makisio mwaka 2018/2019 | Mapato Halisi | Makisio Mwaka 2019/2020 | Mapato Halisi | % hadi Desemba, 2019 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Ushuru wa Machinjio | 28,852,000 | 5,718,400 | 162,000 | | |
| | Mnada wa ng’ombe | 5,400,000 | 4,268,500 | 9,500,000.00 | 0 | 0 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Ushuru wa uvuvi na leseni | 21,005,600 | 7,418,000 | 15,750,000.00 | 7,421,200.00 | 47.1 |
| | Mapato kutokana na ngozi | 1,800,000 | - | | | |
| | Mapato kutokana na mali za Halmashauri | 424,650,000 | 93,515,800 | 332,520,000.00 | 130,530,000.0 | 39.3 |
| | Ushuru wa mazao ya Misitu | 89,900,000 | 68,125,103.24, | 131,650,000.00 | 80,316,964.86 | 39 |
| | Ushuru wa vibali vya matangazo | 10,320,000 | 8,130,000 | 10,320,000 | 9,830,107 | 95 |
| | Mapato ya Ukumbi | 2,400,000 | - | | | |
| | Ushuru wa leseni za vileo | 2,040,000 | 280,000 | 1,400,000 | 440,000 | 31.4 |
| | Ushuru wa stendi ya magari | 70,920,000 | 26,071,200. | 147,095,000 | 29,640,700 | 20.2 |
| | Ushuru wa soko | 1,000,000 | 1,300 | | | |
| | Ushuru wa leseni za biashara | 92,323,000 | 65,502,300 | 90,939,000 | 61,297,271.77 | 67.7 |
| | Kodi ya utoaji wa huduma | 45,568,000 | 16,836,008.69 | 55,360,400 | 16,297,271.77 | 29.4 |
| | Ushuru wa nyumba za kulala wageni | 40,800,000 | 17,630,000 | 45,600,000 | 15,338,000.00 | 33.6 |
| | Ada ya usajili | 1800,000 | - | 4,500,000 | 1,260,000.00 | 28.00 |
| | Mapato Mengineyo | 5,000,000 | 5,088,233.33 | 5,000,000.00 | 2,297,102.14 | 45.9 |
| | Ushuru wa Mahindi | 60,000,000 | 11,903,000 | 30,000,000 | 34,775,400.00 | 115.9 |
| | Ushuru wa Maharage | 50,000,000 | 66,067,400 | 100,000,000.00 | 115,224,799.94 | 115.2 |
| | Ushuru wa meza | 48,720,000 | 43,619,062 | 90,828,000.00 | 700,400.00 | 0.8 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | |
| | Ushuru wa mazao mengine ya biashara | 7,500,000 | 7,819,200 | 7,500,000.00 | 21,763,600.00 | 290.2 |
| | Ushuru wa zabuni | 1,000,000 | 5,450,000 | - | - | - |
| | Ushuru wa maegesho ya magari | 26,000,000 | 7,605,500 | 26,000,000.00 | 9,119,500.00 | 35.1 |
| | Vibali vya ujenzi | 2,700,000 | 3,785,000 | 6,000,000.00 | 4,435,000.00 | 73.9 |
| | Ushuru wa madini ya ujenzi | 5,000,000 | 335,000 | 4,000,000.00 | 390,000.00 | 9.8 |
| | Tozo na faini | 12,000,000 | 1,915,020 | 15,000,000.00 | 5,245,821.00 | 35.0 |
| | Mapato kutoka TFDA | 10,000,000 | 100,000 | 8,300,000.00 | | 0.0 |
| | Ushuru wa Usafi | 10,000,000 | 0 | 15,000,000.00 | 7,602,900.00 | |
| | Ushuru wa Mabango | 0 | 0 | | | |
| | Uuzaji wa Viwanja | 287,500,000 | 0 | 163,717,600.00 | | 0.0 |
| | Kodi ya ardhi | 0 | 0 | | | |
| | Kodi ya majengo | 0 | 0 | | | |

## MAKISIO YA MAKUSANYO YA MAPATO YA NDANI KWA MWAKA 2020/2021

| CHANZO/MAELEZO | IDADI | KIASI @TSH | JUMLA |
|---|---|---|---|
| VIBANDA SOFYA | 300 | 300 X 20,000 (kodi) X12 (miezi) | 72,000,000.00 |
| MEZA ZA ZAMANI SOFYA | 50 | 50x5000x12(Miezi) | 3,000,000.00 |
| MEZA SOFYA | 110 | 110 x 5,000 (kodi) x 12 (miezi) | 6,600,000.00 |
| VIBANDA SOKO KUU MJINI | 358 | 358 x 50,000 (kodi) x 12 (miezi) | 214,800,000.00 |
| VIBANDA STANDI YA MURUSI | 200 | 200x10000x12 | 24,000,000.00 |
| MEZA SOKO KUU MJINI(YEBO) | 20 | 20 x 20000 x 12 | 4,800,000.00 |
| MEZA SOKO KUU MJINI (MCHELE) | 30 | 30 x 15000 x 12 miezi | 5,400,000.00 |
| MEZA SOKO KUU MJINI (DAGAA NA SAMAKI) | 35 | 35 x 10000 x 12 miezi | 4,200,000.00 |
| MEZA SOKO KUU MJINI (MEZA ZINGINEZO ZOTE) | 173 | 173 x 7000 x 12 miezi | 14,532,000.00 |
| RTC A & B | 1 | 650,000 x 12 miezi | 7,800,000.00 |
| MURUSI STENDI KUU BASI MAKUBWA | 10 | 10 x 3000 x 365 siku | 10,950,000.00 |
| MURUSI STENDI KUU BASI MADOGO | 30 | 30 x 1500 x 365 siku | 10,950,000.00 |
| MURUSI STENDI KUU TAX | 10 | 10 x 1000 x 365 siku | 3,650,000.00 |
| STENDI YA HIACE MNARANI | 20 | 20 x 1000 x 365 siku | 10,950,000.00 |
| STAND YA BAJAJ KWA SHAYO | 65 | 65 x 500 x 365 Siku | 11,862,500.00 |
| STENDI YA TAX MNARANI | 30 | 50 x 1000 x 365 siku | 10,950,000.00 |
| STENDI YA TAX MJINI | 40 | 40 x 1000 x 365 | 14,600,000.00 |
| **Jumla ndogo** | | | **431,044,500.00** |
| | | | |
| **LESENI ZA BIASHARA** | | | |
| MADUKA YA REJAREJA | 1201 | 1201 (idadi) x 51,000 (kiwango cha kulipa) | 61,251,000.00 |
| MADUKA YA NUSU JUMLA | 10 | 10 x 201,000 kiwango | 1,005,000.00 |
| MADUKA YA SPEA ZA PIKIPIKI | 30 | 30 x 81,000 kiwango | 2,430,000.00 |
| MADUKA YA SPEA ZA MAGARI | 7 | 7 x 251,000 | 1,757,000.00 |
| MADUKA YA SPEA ZA BAISKELI | 30 | 30 x 31,000 | 930,000.00 |
| MADUKA YA MADAWA | 20 | 20 x 101,000 | 2,020,000.00 |
| MASHINE ZA KUSAGA NA KUKOBOA | 40 | 40 x 31,000 | 1,240,000.00 |
| MADUKA YA VIFAA VYA UMEME | 17 | 17 x 101,000 | 1,717,000.00 |
| NYUMBA ZA KULALA WAGENI | 92 | 92 x 101,000 | 9,292,000.00 |
| VITUO VYA MAFUTA | 15 | 15 x 151,000 | 2,265,000.00 |
| MPESA | 100 | 100 x 51,000 | 5,100,000.00 |
| MADUKA YA MITUMBA | 50 | 50 x 16,000 | 800,000.00 |
| KUNUNUA NA KUUZA MAZAO | 18 | 18 x 101,000 | 1,818,000.00 |
| WORKSHOP/GARAGE | 10 | 10 x 101000 | 1,010,000.00 |
| MADUKA YA VIFAA VYA UJENZI | 20 | 20 x 151,000 | 3,020,000.00 |
| MABUCHA | 20 | 20 x 51,000 | 1,020,000.00 |
| OIL AND LUBLICANT | 15 | 15 x 101000 | 1,515,000.00 |
| **Jumla ndogo** | | | **98,190,000.00** |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **LESENI ZA VILEO** | | | |
| GROSARY NDOGO | 55 | 50 x 20000 kiwango | 1,100,000.00 |
| BAR | 10 | 5 x 40000 | 400,000.00 |
| WHOLESALERS | 5 | 1 x 20000 | 100,000.00 |
| **Jumla ndogo** | | | **1,600,000.00** |
| | | | |
| **USHURU WA NYUMBA ZA KULALA WAGENI** | 92 | 3,800,000.00 | **349,600,000.00** |
| | | | |
| **USHURU WA MAZAO** | | | |
| Maharage | 100000 | 100000 x 2000 | 200,000,000.00 |
| Mahindi | 50000 | 50000 x 2000 | 100,000,000.00 |
| Mihogo Mikavu kwa gunia | 10000 | 10000 x 2000 | 10,000,000.00 |
| Miwa kwa tani | 300 | 300 x 10000 | 3,000,000.00 |
| Mbaazi | 2500 | 2500 x 2000 | 5,000,000.00 |
| Mchele | 2000 | 2000 x 2000 | 4,000,000.00 |
| **Jumla ndogo** | | | **317,000,000.00** |
| | | | |
| **KITENGO CHA MISITU(MBAO)** | | | |
| MBAO | 4,500,000 | 4500,000 x 200 | 90,000,000.00 |
| MIRUNDA | 100000 | 300 | 30,000,000.00 |
| MABANZI | 8000 | 100 | 800,000.00 |
| VITANDA | 50 | 5,000.00 | 250,000.00 |
| FREMU | 100 | 2,000.00 | 200,000.00 |
| MILANGO | 100 | 4,000.00 | 400,000.00 |
| KUSAFIRISHA NGUZO ZA UMEME | TREATED 2000 | 750 x2000 | 1,500,000.00 |
| | NOT TREATED 1000 | 8504 x1000 | 17,008,000.00 |
| **Jumla ndogo** | | | **115,158,000.00** |
| | | | |
| **KITENGO CHA NYUKI** | | | |
| ASALI(KWA NDOO) | 100 | 1,000.00 | **100,000.00** |
| | | | |
| **MIFUGO** | | | |
| Ukaguzi wa nyama Ng'ombe | 4400 | 4400 x2300 | 10,120,000.00 |
| Ukaguzi wa nyama Mbuzi/Kondoo | 3600 | 3600 x1300 | 4,680,000.00 |
| Ukaguzi wa nyama (Nguruwe) | 4300 | 4300 x1000 | 4,300,000.00 |
| Ushuru wa Usafrishaji Ngozi Ng'ombe | 3500 | 3500x300 | 1,050,000.00 |
| Ushuru wa Usafrishaji Ngozi Mbuzi/Kondoo | 3500 | 3500x100 | 350,000.00 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Ushuru wa mazao yauvuvi | 1 | Mwaka | 15,000,000.00 |
| Ushuru wa leseni za kuuza mazao ya uvuvi | 250 | 250x10000 | 2,500,000.00 |
| **Jumla ndogo** | | | **27,080,000.00** |
| **TFDA** | | | |
| MASHINE ZA KUSAGA NA KUKOBOA | 40 | 40 x 50000 kiwango | 2,000,000.00 |
| MADUKA YA REJA REJA | 126 | 126 x 50000 | 6,300,000.00 |
| **Jumla ndogo** | | | **8,300,000.00** |
| | | | |
| **UJENZI** | | | |
| Vibali vya Ujenzi -Makazi | 200 | 20000 | 4,000,000.00 |
| Vibali vya Ujenzi -Biashara | 40 | 50000 | 2,000,000.00 |
| **Jumla ndogo** | | | **6,000,000.00** |
| | | | |
| **ARDHI** | | | |
| Ada ya upimaji wa viwanja | 100 | 50000 | 5,000,000.00 |
| Ada ya maombi ya viwanja | 100 | 20000 | 2,000,000.00 |
| **Jumla ndogo** | | | **7,000,000.00** |
| | | | |
| **USHURU WA MADINI** | | | |
| Mawe | 200 | 10000 | 2,000,000.00 |
| Kokoto | 200 | 5000 | 1,000,000.00 |
| Kifusi | 200 | 5000 | 1,000,000.00 |
| **Jumla ndogo** | | | **4,000,000.00** |
| | | | |
| **MINARA** | | | |
| Ushuru - TIGO | 1 | 8,400,000.00 | 8,400,000.00 |
| Airtel | 1 | 6,000,000.00 | 6,000,000.00 |
| Ushuru - VODA | 1 | 5,520,000.00 | 5,520,000.00 |
| **Jumla ndogo** | | | **19,920,000.00** |
| | | | |
| **USHURU WA KUTOA HUDUMA** | | | |
| **A:VITUO VYA MAFUTA:** | | | |
| 1.Mtokasulu filling station | | 12miezi x 200,000 | 2,400,000.00 |
| 2.Muholeza filling station | | 12miezi x 200,000 | 2,400,000.00 |
| 3.lake oil filling station | | 12miezi x 200000 | 2,400,000.00 |
| 4.Hi Energy | | 12miezi x 210000 | 2,520,000.00 |
| 5.Dual filling station | | 12miezi x 120000 | 1,440,000.00 |
| 6.EAFCO.LTD | | 12miezi x 200000 | 2,400,000.00 |
| 7.Lake Tanganyika | | 12miezi x 200000 | 2,400,000.00 |
| 8.Kitema Filling Station | | 12miezi x 200000 | 2,400,000.00 |
| 9.Bigazi Filling Station | | 12miezi x 50000 | 600,000.00 |
| 10.BRAVA ENERGY LIMITED | | 12miezi x 200000 | 2,400,000.00 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 11.REUBEN KAHUZA FILLING STATION | | 12miezi x 200000 | 2,400,000.00 |
| 12.OMARY KAJICHO FILLING STATION | | 12miezi x 200000 | 2,400,000.00 |
| 13.DUNIA FILLING STATION | | 12miezi x 50000 | 600,000.00 |
| 14.KOMANYA FILLING STATION(BOGWE) | | 12miezi x 50000 | 600,000.00 |
| 15.SENGIYUMVA FILLING STATION | | 12miezi x 50000 | 600,000.00 |
| 16.MUNGU KANIPA FILLING STATION | | 12miezi x 200000 | 2,400,000.00 |
| **Jumla ndogo** | | | **30,360,000.00** |
| **A:MASHIRIKA MBALI MBALI:** | | | |
| 1.NMB | | 12miezi x 464888.67 | 6,530,200.00 |
| 2.CRDB | | 12miezi x 479333.33 | 6,530,200.00 |
| 3.ABC | | 12miezi x 80000 | 960,000.00 |
| 4.Faidika | | 12miezi x 25000 | 300,000.00 |
| 5.BAYPORT | | 12miezi x 25000 | 300,000.00 |
| 6.PLATNUM | | 12miezi x 25000 | 300,000.00 |
| 7.BARAKA FINANCING BANK | | 12miezi x 25000 | 300,000.00 |
| 8.CHAKUWAKA SACCOS | | 12miezi x 25000 | 300,000.00 |
| **Jumla ndogo** | | | **15,520,400.00** |
| **UTAWALA** | | | |
| Ushuru wa maegesho | | | 26,000,000.00 |
| Tozo na Faini | | | 5,000,000.00 |
| Ada ya matangazo | | | 3,000,000.00 |
| **Jumla ndogo** | | | **28,000,000.00** |
| **VYOO** | | | |
| Sofya | 12 | 12 X 30000 | 3,600,000.00 |
| Murusi | 12 | 12 x 30000 | 3,600,000.00 |
| Kumsenga | 12 | 12 x 40000 | 4,800,000.00 |
| | | | **12,000,000.00** |
| | | | |
| **ADA YA VIKUNDI VYA MAENDELEO** | 450 | 450 x 10000 | **4,500,000.00** |
| | | | |
| **JUMLA KUU** | | | **1,475,372,900.00** |

## Matumizi ya Kawaida

Katika Mwaka wa Fedha **2020/2021** Halmashauri imepanga Kukusanya/kupokea kiasi cha Tshs. **1,048,549,800.00**.00 kutoka chanzo cha Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida. Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida ina sehemu mbili yaani, Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida pamoja na Fidia kwa vyanzo vilivyofutwa kama jedwali hapo chini linavyoonesha.

| Na | Chanzo cha Fedha | Bajeti Idhinishwa |
|---|---|---|
| i. | Ruzuku ya Matumizi ya Kawaida | 997,188,800.00 |
| ii. | Fidia kwa vyanzo vilivyofutwa | 51,361,000.00 |
| | **Jumla** | **1,048,549,800.00`** |

**Mishahara (PE)**

Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Halmashauri imekadiria kulipa mishahara kiasi cha Tshs.

| Na | Idara | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Utawala | 1,444,537,500.00 |
| 2 | Elimu Utawala na Watu Watu Wazima | 111,387,000.00 |
| 3 | Elimu Msingi | 11,577,345,000.00 |
| 4 | Elimu ya Sekondari | 4,671,093,000.00 |
| 5 | Afya Tiba | 790,068,000.00 |
| 6 | Afya Kinga | 431,745,000.00 |
| 7 | Vituo vya huduma za afya | 721,353,000.00 |
| 8 | Zahanati | 1,300,605,000.00 |
| 9 | Ujenzi | 110,610,000.00 |
| 10 | Maji | 55,416,000.00 |
| 11 | Watendaji wa Mitaa | 409,837,500.00 |
| 12 | Kilimo | 149,619,000.00 |
| 13 | Mifugo | 66,480,000.00 |
| | Jumla | **21,840,096,000.00** |

**Miradi ya maendeleo.**

Katika Mwaka wa Fedha **2020/2021** Halmashauri ya Mji imepanga kukusanya na kutumia kiasi cha T shs**. 5,753,496,579.32** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Fedha hizo zinategemewa kutoka kwa Wafadhili na Serikali Kuu kama jedwali hapo chini linavyoonesha.

Jedwali ; makadirio ya mapato na matumizi kwa miradi ya maendeleo Mwaka wa Fedha 2020/2021

| Na | Jina la mradi | Kiasi |
|---|---|---:|
| | COUNCIL BUILDING | 1,553,832,910.00 |
| | Jimbo Fund - CDCF | 44,190,000.00 |
| | Health Sector Basket Fund - HSBF | 425,771,846.00 |
| | Multilateral UNICEF | 80,098,200.00 |
| | IMA | 62,610,000.00 |
| | Result Based Financing - RBF | 923,984,873.32 |
| | Global Fund | 8,034,000.00 |
| | Tanzania Health Promotion Support-THPS | 143,886,750.00 |
| | Tanzania Social Action Fund - TASAF | 1,202,910,000.00 |
| | School Meals Grant | 426,276,000.00 |
| | Responsibility Grants | 228,600,000.00 |
| | Capitation Grants-Dev | 455,052,000.00 |
| | Schools Fee Compensation Grants | 198,250,000.00 |
| | **Jumla** | **5,753,496,579.32** |

**MAOMBI MAALUMU**

1. GARI YA MKURUGENZI

## MWELEKEO WA BAJETI YA MWAKA 2020/2021

Halmashauri imepanga kutekeleza shughuli mbalimbali za maendeleo kwa wananchi wa Halmashauri ya Mji Kasulu kama ifuatavyo:-

- Kuendelea na ukamilishaji wa jengo la Halmashauri ya Mji Kasulu ambalo litatumiwa na idara na vitengo vya Halmashauri. Jengo hili kwa sasa lipo hatua ya ujenzi wa box na kusuka nondo kwa ajili ya kupokea ghorofa la tatu. Kiasi cha Tshs. 1,553,832,910.00 kimetengwa katika mwaka wa fedha 2020/2021 kwa ajili ya ukamilishaji wa mradi huo.

- Kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani hasa yasiyo na masharti ambapo kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kiasi cha Tshs.1, 475,372,900.00 kinategemewa kukusanywa.

- Kuendelea kusimamia utoaji wa elimu bila malipo ambapo kiasi cha Tshs. 1,308,178,000.00 kimetengwa kwa ajili ya shule zote za msingi na sekondari

- Kutenga asilimia 10 ya mapato ya Ndani kwa ajili ya utoaji mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana na walemavu ambayo kwa mwaka wa Fedha 2020/2021 ni 147,537,290
- Vitambulisho vya wazee kwa ajili ya matibabu vimezingatiwa katika bajeti hii.

- Utunzaji wa mazingira kwa kulinda vyanzo vya maji na uoteshaji miti umezingatiwa

- Kurasimisha makazi holela kwa viwanja katika kata za Kumsenga, Kimobwa na Mwilamvya

- Kuandaa michoro ya Mipango miji katika eneo la Kinkati na Mubondo

- Kuendelea kuimarisha huduma za afya zinazotolewa katika Halmashauri ya Mji Kasulu

- Miradi ya uboreshaji huduma za maji na miundombinu ya barabara imewasilishwa kwa mamlaka husika.

- Kuendelea kuimarisha huduma za afya kwa kutenga fedha katika bajeti ikijumuisha pia ununuzi wa dawa kulingana na maelekezo na mahitaji yaliyopo.

## MAKISIO YA WATUMISHI KUPANDA VYEO, KUBADILISHIWA MUUNDO NA AJIRA MPYA KWA BAJETI 2020/2021

| | IDARA | KUPANDA VYEO | KUBADILI MUUNDO | AJIRA MPYA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Utawala | 17 | 7 | 85 |
| 2. | Elimu Utawala | 4 | - | - |
| 3. | Elimu Msingi | 853 | 124 | 200 |
| 4. | Elimu sekondari | 269 | - | 90 |
| 5. | Afya Tiba | 24 | 2 | 14 |
| 6. | Afya kinga | 11 | - | 40 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 7. | Kituo cha Afya | 50 | 3 | 33 |
| 8. | Zahanati | 71 | 4 | 30 |
| 9. | Ujenzi | 2 | - | 7 |
| 10. | Maji | 1 | - | - |
| 11. | Mtaa(watendaji) | 10 | - | 92 |
| 12. | Kilimo | 7 | - | 24 |
| 13. | Mifugo | 1 | 2 | 4 |
| | **JUMLA** | **1320** | **142** | **619** |

Mapendekezo ya bajeti yameambatishwa.